



# THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA

**A. M. E. C. E. A**

**MAIN EXAMINATION**

**SEPTEMBER – DECEMBER 2020**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII**

**IDARA YA KISWAHILI, LLC**

**MPANGO WA MCHANA**

**KIM 420: UANDISHI WA MAKALA MAALUM NA MAKALA YA KIPEKEE**

P.O. Box 62157  
00200 Nairobi - KENYA  
Telephone: 891601-6  
Ext 1022/23/25  
Fax: 254-20-891084  
email: [det@cuea.edu](mailto:det@cuea.edu)  
[exams@cuea.edu](mailto:exams@cuea.edu)  
[directorofexams@cuea.edu](mailto:directorofexams@cuea.edu)

<b>Date: DESEMBA 2020</b>	<b>Muda: SaaMbili</b>
<b>Maagizo: Jibuswali la KWANZA namengine MAWILI</b>	

- (a) Fafanua dhana ya makala. (alama 2)
- (b) Eleza kategoria nne za makala maalum (alama 8)
- (c) Soma makala haya na ujibu maswali.

## **ChikichiAuawaKinyama**

Maandamano yalizunguka mtaa mzima kasha yakaelekea nyumbani kwa Chikichi. Alipo sikia nyimbo zakulilia damu yake, alikomelea kwa ndani. Nao,

Hawakutaka kufunguliwa. Alisikia vile walikuwa wanatingisha mlango na kuta za jingo hilo.

Akajuafika kuwa hawakutishwa na kujifungia kwake. Aliamua kufungua mwenyewe.

Wakamvuta nje.

Wakakataa kusikia chochote kutoka kwake. Wakakataa kusikia msalimemtume zake au msalie nani. Wakamtwanga kama mahindi kinuni. Akajitupa huku na kule. Akajaribu kutoroka. Umati ukawa naye pua na mdomo. Wakabururana hadi pale kwenye *Chachu Road*. Katika eneo ambako Bwana Kambare alikuwa ameokotwa akiwa mzoga. Mwanamke mwenye kisasi aliokota jiwe kubwa kusikojulikanana kumwangushia Chikichi kichwani ubongo mweupe ukatapakaa kwenye lami nyeusi.

Kabla apumue mara ya mwisho alijaribu kuinua mikono, labda atubu dhambi zake lakini alikuwa amechelewa. Akavalishwa pete mbili, moja shingoni na nyingine mapajani. Kama hayo mapaja ndiyo yalikuwa yakimringisha, basi waliamua kuyapaka rangi nyeusi. Akanyunyiziwa cha kunyunyiziwa mwili mzima. Basi.

Moto ukaja juu kuliko wa kifuu. Hawakutaka sheria wala amri yoyote kuchukua usukani. Hawakutaka polisi wafike wachukue hatua kwani hatua zao walizopenda kuzichukua zilijulikana. Mathalani, kutoka wakati kesi ya Bwana Kambare iliporipotiwa walikuwa wamefanya nini? Hakuja tokea chochote.

Hakuna mshukiwa ambaye aliweza kukamatwa. Hakuna upelelezi wowote ambao walifanya wala kuita waliotajwa kuwa washukiwa kuandikisha taarifa zozote. Ilishangaza kuwa hawakujua ni wapi angepatikana Chikichi ilhali wao wananchi walikuwa wanajua. Hawakutaka afike mbinguni aanze kumsumbua Mungu au hata shetani.

Ati huyu aende jahanamu akachomekee huko. Hapana. Malipo ni papa hapa duniani. Akhera yaenda hesabu tu. Alilipia yake. Alichomeka kwa moto wa jahanamu humu duniani. Hakuhitaji kwenda kuchomekea kwingine.

- (i) Tambua na utolee mifano sifa za makala bora katika makala uliyosoma. **(alama 10)**
- (ii) Ikiwa makala uliyosoma yangukuwa ya kuchapishwa kwenye gazeti, eleza vipengele muhimu ambavyo vingehitajika ongezwa. **(alama 10)**

2(a) Fafanua njia tano ambazo kwazo mtu anaweza kupevusha usomaji wake wa makala. **(alama 10)**

(b) 'Kuna mikakati mbalimbali ya usomaji wa makala.' Jadili mitano. **(alama 10)**

3. Eleza vile mambo yafuatayo yanavyoathiri uandishi wa makala.

(a) Hadhira lengwa

(b) Mada

(c) Mwandishi **(alama 20)**

4. (a) 'Uandishi wa makala ni mchakato unaozingatia hatua kadha muhimu.' Thibitisha.

**(Alama 10)**

(b) Eleza majukumu ya vyombo vya habari katika uandishi na usambazaji wa makala maalum. **(Alama 10)**

5. 'Mitandao ya kijamii imebadili pakubwa uandishi wa makala katika siku za hivi karibuni.' Jadili kauli hii huku ukibainisha uzuri na ubaya wa mitandao hii. **(Alama 20)**

**\*MWISHO\***

---

CUEA/ACAD/EXAMINATIONS/DIRECTORATE OF EXAMINATIONS & TIMETABLING Page 3

***ISO 9001:2015 Certified by the Kenya Bureau of Standards***